# SIGNS AND TOKENS

## ISHARA NA VITENDO VYA IMANI VYENYE KUZALISHA MATOKEO

**Pastor Tony Osborn**

**© May 2024 Pastor Tony Osborn**

Kitabu hiki kimeandikwa na **PASTOR TONY OSBORN**. Haki zote zimehifadhiwa, huruhusiwi kunakili, kurudufu au kutumia sehemu ya kitabu hiki bila idhini ya mwandishi.

Kufanya hivyo itakuwa ni Ukiukwaji wa taratibu na hii inaweza kukupelekea kushtakiwa kutoka kwa waandaaji wa kazi hii.

**Pastor, Tony Osborn**

**Dar es salaam, TANZANIA (Afrika Mashariki)**

**Simu: 0762153539/0659085731**

**Instagram / Tiktok: Pastor Tony Osborn**

**ISBN: 978-99112-9811-5-**7

Kwa Ajili Yako.
**(Present to you)**

Kutoka Kwa.
**(From)**

# YALIYOMO:

**SHUKRANI.** ........................................................ **ix**

**UTANGULIZI.** ..................................................... **xi**

KUSUDI LA KUANDIKA KITABU HIKI. ............. xx

***Sura ya Kwanza.*** ........................................... ***1***

TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA MCHANGA/ UDONGO ......................................... 1

MAOMBI YA KUFUKUA CHOCHOTE CHA KWETU KILICHOMEZWA NA KUZIKWA NA ARDHI. ......................................................... 9

MAOMBI YA KUPANDA MBEGU NJEMA JUU YA ARDHI NA KUIAMURU KUTII YALE YOTE UTAKAYOYATUMA. .................................. 12

MAOMBI YA UKIRI JUU YA ARDHI. ...................... 14

***Sura ya Pili.*** ................................................... ***16***

TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA MAJI. ........... 16

MAOMBI YA KUYAOMBEA MAJI KUWA DAMU YA YESU INENAYO MEMA. ................... 24

MAOMBI YA KUTENGA VITU VYAKO KWA KUTUMIA DAMU YA YESU ................................. 25

MAOMBI YA UKIRI JUU YA MAOMBI ULIYOFANYA KWA KUTUMIA DAMU YA YESU ............................................................... 28

***Sura ya Tatu....................................................29***

TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA KARATASI.............................................................. 29

MAOMBI YA KUFUTA NA KUAHIRISHA TAARIFA NA HABARI ZOTE MBAYA. ...............40

MAOMBI YA KULETA HABARI NA TAARIFA NZURI KATIKA MAISHA YETU ....................... 43

MAOMBI YA KUWATANGAZIA WATU WOTE WALIOPANGA KUTUANDIKIA BARUA ZENYE HABARI MBAYA. ....................................45

MAOMBI YA UKIRI KWA TENDO LA IMANI TULILOFANYA KWA KUTUMIA KARATASI. ........................................................... 54

***Sura ya Nne. ...................................................55***

TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA MAKUFULI............................................................ 55

MAOMBI YA KUFUNGUA KILA KIFUNGO KILICHOKUSHIKILIA....................................... 59

MAOMBI YA KUFUNGA KILA HALI MBAYA NA MAMBO MABAYA MAISHANI MWETU......63

MAOMBI YA UKIRI KWA TENDO LA IMANI TULILOFANYA KWA KUTUMIA MAKUFULI 66

***Sura ya Tano...................................................67***

TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA CHUMVI NA MAFUTA. ........................................................ 67

Namna ambavyo Chumvi hutumika ulimwengu wa Roho ............................................................... 67
Namna ambavyo mafuta hutumika ulimwengu wa Roho ............................................................... 69

MAOMBI KWA KUTUMIA CHUMVI...................73

MAOMBI KWA KUTUMIA MAFUTA. .................75

MAOMBI YA UKIRI KWA TENDO LA IMANI TULILOFANYA KWA KUTUMIA CHUMVI NA MAFUTA. ........................................77

***Sura ya Sita........................................................ 78***

TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA JIWE. ......... 78

***Sura ya Saba...................................................... 83***

TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA MSHUMAA. ........................................................... 83

MAOMBI YA KUWASHA TAA ZETU ILI ZIANGAZE. ......................................................... 88

MAOMBI YA UKIRI KWA TENDO LA IMANI TULILOFANYA KWA KUTUMIA MSHUMAA. ....................................................... 90

***Sura ya Nane. ................................................ 91***

TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA UPEPO...... 91

***Sura ya Tisa. ..................................................94***
TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA KIATU.......94

MAOMBI YA IMANI KWA KUTUMIA VIATU NA MIGUU YETU..................................98

MAOMBI YA UKIRI KUPITIA TENDO LA IMANI LA KIATU TULILOFANYA;. ................100

**HITIMISHO:........................................................ 101**

# SHUKRANI:

Ninamshukuru Mungu sana kwa uaminifu wake na kwa kunijalia ROHO MTAKATIFU ambaye kwa mafunuo yasiyo ya kawaida amenipa NEEMA ya kuandika kitabu hiki kilichobeba mafunuo na siri nyingi sana juu ya somo zima la ishara na vitendo vya kiimani ambavyo vinaweza kubadilisha maisha ya mtu.

Siri zilizoandikwa humu kwa uwezo wa Roho wa Mungu zitakusaidia na kukuongoza hatua kwa hatua namna ya kutumia ishara na matendo ya kiimani yaliyomo humu ili kupata ukombozi katika kila eneo la maisha yako na kuweza kukuinua katika ukuu ambao Mungu alikuita.

Neno la Mungu linasema katika kitabu cha;

**Marko 16:17-18**

**“Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio; kwa jina langu watatoa pepo; watasema kwa lugha mpya; watashika nyoka; hata wakinywa kitu cha kufisha, hakitawadhuru kabisa; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya.”**

Kwahiyo ishara na matendo ya kiimani sio jambo jipya bali ni jambo ambalo Yesu mwenyewe aliliruhusu kwetu ili kuweza kuona na kupata matokeo tunayoyatamani maishani mwetu.

Kitabu hiki ni mkusanyiko wa mafunuo wa mafundisho ya Kiimani ambayo yatatuhusisha sisi kufanya vitendo vya kiimani kwa kutumia vitu ambavyo Mungu mwenyewe aliviumba ili kuleta matokeo katika maisha yetu.

Kama vile Neno la Mungu linavyosema katika kitabu cha;

**Yakobo 2:7**

**"Vivyo hivyo, imani peke yake bila matendo imekufa."**

Kwahiyo ili imani zetu ziwe na matokeo lazima ziambatane na matendo. ***Matendo gani?*** Utajifunza zaidi katika kitabu hiki.

Shukrani zangu za pekee ziwafikie watoto wangu wa kiroho wote, ndani na nje ya nchi ya Tanzania, kwa kunipenda, kuniombea na zaidi ya yote kunipokea na kuniamini na kwa Kumuamini Mungu aliyeniita na huduma iliyopo ndani yangu.

Ninawashukuru sana kwa kuwa nyie mmenipa nafasi katika mioyo yenu na kuamini kile kitu na huduma Mungu ameweka ndani yangu.

Ninawapenda, ninawaombea na Mungu wa mbinguni awabariki sana.

Kiupekee kabisa ninamshukuru mke wangu mpenzi Mrs Neema Tony Kapola ambaye amekuwa akikesha pamoja nami, akisukuma na kusimamia kwa ufasaha ukamilifu wa kitabu hiki. Ninakupenda na Asante kwa kusimama na mimi katika wito na kazi hii ambayo Mungu amenipa.

Mungu aendelee kukuonekania wewe na familia yako ndani ya mwaka huu.

Amen……………………

**-Pastor Tony Osborn**

# UTANGULIZI:

Katika Biblia tunaziona na kuzisoma habari za manabii, mitume na watumishi mbalimbali wa Mungu na moja ya kitu kikubwa kilichotawala katika kipindi hiko ni ishara na vitendo vya Kiimani ambavyo katika hivyo jina la Mungu lilitukuzwa sana.

Ishara na vitendo vya imani vilivyofanyika ilikuwa ni njia mojawapo ya kumtambulisha Mungu ndani ya maisha ya mtu.

Namaanisha, kutokana na zile ishara na matendo ya imani yaliyofanyika watu waliweza kumjua Mungu na kuamini uwepo wake.

Kila kitendo cha imani kilichofanyika kilipelekea Mungu kusifiwa na kujulikana na wale wasiokuwa wamemjua au kumuamini.

Kabla sijaelezea kiundani sababu au kusudi la kuandika kitabu hiki, tuangalie mifano michache ya watu wa Mungu katika Biblia ambao walifanya vitendo vya kiimani na ishara ambazo zilifanya Mungu atukuzwe na kuogopwa na wao kufanikiwa.

i. **Eliya (Aliizuia Mvua kunyesha na Manabii wa Baali)**

Kwanza kabisa, tunaona habari ya Eliya na namna ambavyo alizuia mvua kunyesha isipokuwa kwa neno lake.

Tunasoma katika kitabu cha;

**1 Wafalme 17:1-2**

**“Basi Eliya wa kijiji cha Tishbe huko Gileadi, akamwambia mfalme Ahabu, “Ninaapa kwa Mwenyezi-Mungu, Mungu wa Israeli aliye hai ambaye mimi ninamtumikia: Hakutakuwa na umande wala mvua mpaka nitakapotoa amri.”**

Hakuna mtu anayeweza kuamuru mvua kutokunyesha isipokuwa ana nguvu au mamlaka ya kufanya hivyo au amepewa nguvu na mamlaka ya kufanya hivyo na Mungu mwenyewe.

Hii inaonyesha kuwa; nabii Eliya alipewa nguvu na mamlaka ya kutiisha hali ya hewa kufata na kutii kile alichokitamka yeye na sio mtu mwingine na matokeo yake tunaona kuwa aliweza kufanya mvua isinyeshe kwa muda wa miaka mitatu na nusu mpaka pale yeye tena alivyokwenda kujionyesha na kuomba tena mvua inyeshe juu ya nchi.

Hii ni uthibitisho ya kuwa; **“Hata sisi tunaweza kupewa mamlaka juu ya hali ya hewa na vitu vilivyopo duniani kututumikia”**

Pili, Tunaona namna ambavyo Eliya alifanya tendo la imani la kuwakusanya manabii wa Baali na kuwaamuru kuomba kwa mungu wao na yeye aombe kwa Mungu wake na yule atakayejibu kwa moto ndiye atakuwa Mungu wa kweli. Ukisoma vizuri na kuitafakari vizuri hii historia utaona ni kwa namna gani Eliya alifanya tendo kubwa la kiimani.

Nina uhakika Eliya alikuwa na imani kubwa juu ya Mungu wake na alikuwa anaamini kuwa Mungu anaweza kushusha moto ukawaramba wale manabii wa Baali lakini ilibidi afanye tendo la kiimani ambalo lingewafanya wale manabii wa Baali waamini katika Mungu wa mbinguni.

Jaribu kufikiria; ni kwanini Eliya alimwaga mapipa ya maji? Kwanini asingeweka tu kuni kavu na sadaka yake?

Hii inaonyesha kuwa alikuwa anafanya tendo la kiimani ambalo lingemdhihirisha Mungu wake kuwa ni Mungu wa kweli na anayejibu kwa moto.

Tunasoma katika kitabu cha;

**1 Wafalme 18:22-40 "Kisha Eliya akawaambia, "Ni mimi peke yangu nabii wa** Bwana **aliyebaki, lakini Baali ana manabii mia nne na hamsini.**

**Leteni mafahali wawili. Wao na wajichagulie mmoja, wamkate vipande vipande na waweke juu ya kuni lakini wasiiwashie moto. Nitamwandaa huyo fahali mwingine na kumweka juu ya kuni lakini sitawasha moto.**

**Kisha mliitie jina la mungu wenu, nami nitaliitia jina la Bwana Mungu yule ambaye atajibu kwa moto, huyo ndiye Mungu."**

**Kisha watu wote wakasema, "Hilo unalosema ni jema."**

**Eliya akawaambia manabii wa Baali, "Chagueni mmoja kati ya hawa mafahali na mwe wa kwanza kumwandaa, kwa kuwa ninyi mko wengi sana. Liitieni jina la mungu wenu, lakini msiwashe moto." Kwa hiyo wakamchukua yule fahali waliyepewa, nao wakamwandaa.**

**Kisha wakaliitia jina la Baali kutoka asubuhi hadi adhuhuri, wakapiga kelele, "Ee Baali, utujibu!" Lakini hapakuwa na jibu; hakuna aliyejibu. Nao wakacheza kuizunguka madhabahu waliyoijenga.**

**Wakati wa adhuhuri, Eliya akaanza kuwadhihaki, akisema, "Pigeni kelele zaidi! Hakika yeye ni mungu! Labda amezama katika mawazo mazito, au ana shughuli nyingi, au amesafiri. Labda amelala usingizi mzito, naye ni lazima aamshwe."**

**Kwa hiyo wakapiga kelele zaidi na kama ilivyokuwa desturi yao wakajichanja wenyewe kwa visu na nyembe, mpaka damu ikachuruzika. Adhuhuri ikapita, nao wakaendelea na utabiri wao wa kiwazimu mpaka wakati wa dhabihu ya jioni. Lakini hapakuwa na jibu, hakuna aliyejibu, hakuna aliyeangalia.**

**Kisha Eliya akawaambia watu wote, "Sogeeni karibu nami." Watu wote wakamkaribia, naye akakarabati madhabahu ya** Bwana, **ambayo ilikuwa imevunjwa.**

**Eliya akachukua mawe kumi na mawili, moja kwa ajili ya kila kabila la wana wa Yakobo, ambaye neno la Bwana lilimjia, likisema, "Jina lako litakuwa Israeli." Kwa mawe hayo, akajenga madhabahu katika jina la Bwana, na akachimba handaki kuizunguka, ukubwa wa kutosha vipimo viwili vya mbegu. Akapanga kuni, akamkata yule fahali vipande vipande na kuvipanga juu ya kuni. Kisha akawaambia, "Jazeni mapipa manne maji na kuyamwaga juu ya sadaka ya kuteketezwa na juu ya kuni." Akawaambia, "Fanyeni hivyo tena." Nao wakafanya hivyo tena.**

**Akaagiza, "Fanyeni kwa mara ya tatu." Nao wakafanya hivyo kwa mara ya tatu. Maji yakatiririka kuizunguka madhabahu na hata kujaza lile handaki.**

**Wakati wa kutoa dhabihu ya jioni, nabii Eliya akasogea mbele na kuomba, akisema: "Ee** Bwana, **Mungu wa Abrahamu, na Isaki na Israeli, ijulikane leo kwamba wewe ndiye Mungu katika Israeli na ya kwamba mimi ni mtumishi wako na nimefanya mambo haya yote kwa neno lako. Unijibu mimi, Ee** Bwana, **nijibu mimi, ili watu hawa wajue kwamba wewe, Ee** Bwana, **ndiwe Mungu, na kwamba unaigeuza mioyo yao ikurudie tena."**

**Kisha moto wa** Bwana **ukashuka na kuiteketeza ile dhabihu, zile kuni, yale mawe, ule udongo, na pia kuramba yale maji yaliyokuwa ndani ya handaki.**

**Wakati watu wote walipoona hili, wakaanguka kifudifudi na kulia, "Bwana: yeye ndiye Mungu! Bwana: yeye ndiye Mungu!"**

**Kisha Eliya akawaamuru, "Wakamateni hao manabii wa Baali. Msimwache hata mmoja atoroke!" Wakawakamata, naye Eliya akawaleta mpaka Bonde la Kishoni na kuwachinja huko."**

Huyu ni mtu wa kwanza ambaye tumeona ni kwa namna gani alifanya matendo makubwa ya kiimani katika kumdhihirisha Mungu wake.

**ii. Joshua (Alisimamisha Jua)**

Tunasoma katika kitabu cha;

**Joshua 10:12-15**

**"Wakati Mwenyezi-Mungu alipowatia Waamori mikononi mwa Waisraeli, Yoshua alimwomba Mwenyezi-Mungu mbele ya Waisraeli wote, akasema,**

**"Wewe jua, simama kimya juu ya Gibeoni, wewe mwezi, katika bonde la Aiyaloni."**

**Jua likasimama kimya na mwezi ukasimama mpaka taifa la Israeli lilipolipiza kisasi maadui wake. Kama alivyoandika katika kitabu cha Yashari, jua lilisimama kimya katikati ya mbingu, likakatiza safari yake ya kwenda kutua kwa siku nzima.**

**Siku kama hiyo haijawahi kuwako kamwe wala haijapata kuonekana tena, siku ambayo Mwenyezi-Mungu amemwitikia binadamu kwa namna hiyo; maana Mwenyezi-Mungu mwenyewe aliwapigania Waisraeli."**

Kama Joshua alipewa kibali cha kusimamisha jua na mwezi hata wakashinda vita zao hata sisi tukiomba Mungu anaweza kutupa nguvu juu ya vitu na tukavitiisha na vikatutii na sisi tukapata ushindi wetu.

**iii. Musa (Alitumia fimbo kufanya ishara na maajabu)**

Mtu wa tatu tunamuona Musa na namna ambavyo aliitumia fimbo yake kutenda ishara na maajabu lakini pia kufanya kitendo cha kiimani cha kutumia fimbo kugawanya bahari ya shamu na hata wanaisraeli wakapita.

Wakati Musa alikuwa akiiona kama fimbo, Mungu alikuwa anaona kitu ambacho kina uwezo wa kufanya maajabu kwa neno lake.

Fimbo ileile iliweza kugeuka kuwa nyoka, fimbo ileile iliyapiga maji na ikafanya yageuke kuwa damu, na fimbo ileile ndiyo iliyoigawanya bahari ya shamu.

Hii inaonyesha kuwa; kama Mungu alitumia fimbo kuwapa ushindi wanaisraeli hata Farao akawaachia, anaweza kutumia na udongo, anaweza kutumia na maji na vyote vilivyomo duniani sawasawa na vile apendavyo.

Kwahiyo hata wewe unaweza kutumia chochote kinachokuzunguka kufanya matendo ya kiimani sawasawa na ufunuo wa Mungu aliokupa.

### iv. Elisha (Alitumia chumvi kuiponya nchi)

Tunasoma katika kitabu cha;

**2 Wafalme 2:19-22**

**“Baadaye watu wa Yeriko walimwendea Elisha, wakamwambia, “Bwana, kama uonavyo mji huu ni mzuri, lakini maji tuliyo nayo ni mabaya na yanasababisha mimba kuharibika.”**

**Elisha akawaambia, “Tieni chumvi ndani ya bakuli jipya, kisha mniletee.” Nao wakamletea.**

**Elisha akaenda kwenye chemchemi ya maji, akatupa chumvi hiyo ndani na kusema, “Mwenyezi-Mungu asema hivi: Nimeyafanya maji haya kuwa yenye kufaa; tangu sasa hayatasababisha vifo au kutoa mimba.” Na maji hayo yamekuwa ya kufaa mpaka leo, kama alivyosema Elisha.”**

Kwanini Elisha alitumia chumvi kuyaponya maji ya mji ule?

Ni nani alimwambia Elisha anaweza kuiongelesha chumvi na kuiambatanisha na maneno na ikafanya kitu kilekile alichokiamuru?

Hii ni ishara ya kuwa Mungu ametupa uwezo wa kutumia chochote kilichopo duniani kwa ajili ya manufaa yetu na wengine.

Hebu angalia, chumvi kidogo katika bakuli imeweza kutumika kuokoa mji mzima ambao ulikuwa unazaa mapooza kwa sababu ya maji mabaya ya ule mji.

Je, wewe unaweza kutumia nini ambacho ukikiambatanisha na neno la Mungu kitakutii na kufanya yale uliyoyaamuru?

### v. Yesu (Alitumia mate na matope kumponya mgonjwa wa upofu)

Mfano mwingine mzuri ni kutoka kwa Yesu mwenyewe. Tunaona katika Biblia wapo vipofu ambao aliwagusa tu wakapona, wako ambao waliombewa na Yesu na wakapona lakini kuna mmoja ambaye Yesu alitumia mate na udongo na kisha kutengeneza tope na kumpaka kipofu machoni naye akapata kuona tena.

Tunasoma katika kitabu cha:

**Yohana 9:1-9**

**“Yesu alipokuwa akipita, alimwona mtu aliyekuwa kipofu tangu kuzaliwa.**

**Wanafunzi wake wakamwuliza, “Bwana, ni nani aliyetenda dhambi ya kusababisha mtu huyu azaliwe kipofu, ni yeye au wazazi wake?”**

**Yesu akawajibu, “Huyu hakuzaliwa kipofu kwa sababu yeye au wazazi wake walitenda dhambi. Jambo hili lilitokea ili nguvu za Mungu zionekane zikifanya kazi katika maisha yake.**

**Yatupasa tutende kazi yake yeye aliyenituma wakati bado ni mchana kwa maana usiku unakuja ambapo hakuna mtu awezaye kufanya kazi. Wakati nipo ulimwenguni, Mimi ni nuru ya ulimwengu.”**

**Baada ya kusema haya, akatema mate kwenye udongo aka tengeneza tope kwa mate yake akampaka yule kipofu machoni. Kisha akamwambia, “Nenda kanawe uso katika kijito cha Siloamu.” Neno ‘Siloamu’ maana yake ni ‘aliyetumwa.’ Yule kipofu akaenda akanawa na akarudi akiwa anaona!”**

Sasa kwanini Yesu alitumia udongo na mate? Hakuna ajuaye ila inaonyesha ya kuwa unaweza ukatumia chochote ambacho ni uumbaji wa Mungu kukuletea matokeo katika maisha yako.

Ukisoma zaidi katika Biblia utakutana na historia nyingi zaidi za watu wa Mungu na namna ambavyo wao walitumia vitu na kuvitiisha na kuwatumikia wao.

Nimeandika hizi chache ili kukuonyesha kuwa haya unayoenda kuyasoma na kuyafanya sio mambo mapya na wala sio vitu vipya duniani.

Hata watumishi wa zamani walitumia chumvi, walitumia mafuta, wako waliotumia mawe nk. kulingana na mafunuo waliyoyapata kwahiyo utakapokutana na vitendo vya imani vinavyokutaka utumie karatasi au chumvi au udongo usione ni kama kitu kipya bali ufanye kwa imani na uone namna ambavyo vitakuletea matokeo katika maisha yako.

## KUSUDI LA KUANDIKA KITABU HIKI:

Kitabu hiki nimekiandika nikiwa na kusudi la kuwasaidia watoto wa Mungu kuziambatanisha imani zao na vitendo ili ziwaletee matokeo halisi.

Nimegundua kuwa watu wengi hasa waliookoka wana Imani kubwa sana lakini kwa sababu ya kushindwa kuambatanisha imani zao na matendo basi wanabakia kuamini pasipo kuona matokeo ya imani zao.

Mfano; Kama unaamini utapata kazi katika kampuni fulani ni matendo gani uyafanye ili kuonyesha kweli wewe umeamini?

Kama unaamini utaolewa, nini ufanye kitakachoonyesha ulimwengu wa roho kuwa kweli wewe umeamini?

Malaika hawatendei kazi maneno yako ya imani au machozi yako unayolia yanayoonyesha kuwa umeamini. Bali hufanyia kazi vitendo vinavyoambatana na imani yako.

Yaani, kusema una imani au kuamini peke yake haitoshi bali inakuhitaji wewe uambatanishe imani yako na matendo ili kuona matokeo.

Neno la Mungu linasema katika kitabu cha:

**Yakobo 2: 14-23**

**“Ndugu zangu, kuna faida gani mtu kusema ana imani, lakini haonyeshi kwa vitendo? Je, hiyo imani yawezaje kumwokoa?**

**Tuseme kaka au dada hana nguo au chakula.**

**Yafaa kitu gani nyinyi kuwaambia hao: "Nendeni salama mkaote moto na kushiba," bila kuwapatia mahitaji yao ya maisha?**

**Vivyo hivyo, imani peke yake bila matendo imekufa.**

**Lakini mtu anaweza kusema: "Wewe unayo imani, mimi ninayo matendo!" Haya! Nioneshe jinsi mtu anavyoweza kuwa na imani bila matendo, nami nitakuonesha imani yangu kwa matendo yangu.**

**Je, wewe unaamini kwamba yuko Mungu mmoja? Sawa! Lakini hata pepo huamini hilo, na hutetemeka kwa hofu.**

**Mpumbavu wee! Je, wataka kuoneshwa kwamba imani bila matendo imekufa?**

**Je, Abrahamu babu yetu alipataje kukubaliwa kuwa mwadilifu? Kwa matendo yake, wakati alipomtoa tambiko mwanawe Isaka juu ya madhabahu.**

**Waona, basi, kwamba imani yake iliandamana na matendo yake; imani yake ilikamilishwa kwa matendo yake.**

**Hivyo yakatimia yale Maandiko Matakatifu yasemayo: "Abrahamu alimwamini Mungu, na kwa imani yake akakubaliwa kuwa mtu mwadilifu; na hivyo Abrahamu akaitwa rafiki ya Mungu."**

Neno la Mungu limeweka wazi kabisa kuwa Imani bila matendo imekufa na imani ya mtu inakamilishwa kwa matendo.

Hivyo, bila matendo imani yako ni bure.

Kwahiyo sababu ya kwanza iliyonifanya kuandika hiki kitabu ni kuwafundisha watoto wa Mungu namna ya kufanya matendo

yanayoambatana na imani zao ili waweze kuona matokeo ya yale waliyoamini.

Yaani, mpaka unamaliza hiki kitabu utajua nini unatakiwa kufanya kama umemwamini Mungu juu ya kazi sehemu fulani, au ni nini ufanye pale unapomwamini Mungu juu ya uponyaji.

Sababu nyingine iliyonifanya kuandika kitabu hiki ni kuwafundisha na kuwaonesha watoto wa Mungu namna ya kutumia vitu vinavyokuzunguka kukuletea matokeo.

Yaani, utatumiaje maji, mafuta, chumvi au chochote ambacho utakiambatanisha na neno la Mungu kukuletea matokeo katika maisha yako.

Hii ni kwa sababu, sio kila muda wote unaweza ukapata kuwa karibu na mchungaji au nabii, ili ikitokea siku unahitaji msaada wa kiroho wa haraka uweze kujisaidia mwenyewe bila kumtegemea Mchungaji na huu ndio ukuaji wa kiroho.

Kama unaweza kuchukua maji aliyoyaombea mtumishi wa Mungu na yakakusaidia na kukuletea matokeo basi siku akiwa hayupo wewe mwenyewe unaweza ukachukua maji na kuyaombea na yakakuletea matokeo yaleyale uliyokuwa unategemea.

Sasa najua wapo watu watakaouliza, wapi iliandikwa katika Biblia kuwa tunaweza kutumia maji au chumvi au udongo na ukatuletea matokeo.

Kwanza kabla sijakuonyesha andiko lolote nataka ujue kuwa watu wa ulimwengu wa giza wanafanikiwa sana kwa sababu wanatumia sheria hizi za kiroho. Mtu anayeenda kuroga huwa anaroga kwa kutumia vitu.

**Mfano:** Kama anataka kuua vipawa vyako na vipaji vyako au chochote ulichokuwa nacho ataambiwa kabisa achimbe kaburi, atengeneze kinyago ambacho kitaashiria ni wewe na wengine huenda mbali zaidi wanaweza kuchonga kinyago kinachofanana na wewe au hata kuchukua picha yako kisha wanaenda katika lile kaburi walilochimba na kukuzika huku wakitamka maneno yao.

Kama watu wa duniani wanatumia udongo, makaratasi, upepo, vinyago kuturoga na kuharibu maisha yetu sisi pia tunaweza kutumia vitu hivyohivyo kutengeneza maisha yetu.

Tunasoma katika kitabu cha;

**Mwanzo 1:26-31**

**“Kisha Mungu akasema, “Tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; atawale samaki wa baharini, ndege wa angani, wanyama wa kufugwa, dunia yote na viumbe vyote vitambaavyo.”**

**Basi, Mungu akaumba mtu kwa mfano wake; naam, kwa mfano wake Mungu alimuumba. Aliwaumba mwanamume na mwanamke.**

**Mungu akawabariki na kuwaambia, “Zaeni muongezeke, mkaijaze nchi na kuimiliki; muwatawale samaki wa baharini, ndege wa angani, na kila kiumbe hai kitembeacho duniani.”**

**Kisha Mungu akasema, “Tazama, nawapeni kila mmea duniani uzaao mbegu, na kila mti uzaao matunda yenye mbegu; mbegu zao au matunda yao yatakuwa chakula chenu.**

**Nao wanyama wote duniani, ndege wote wa angani, viumbe vyote vitambaavyo, naam, kila kiumbe chenye uhai, chakula chao kitakuwa majani yote ya mimea." Ikawa hivyo."**

Mungu alitupa mamlaka ya kumiliki na kutawala vyote vilivyomo duniani. Maana yake, ukitaka kutiisha chochote juu ya nchi unaweza maana Mungu amekupa hivyo.

Lakini ukiachana na hiyo tunasoma tena katika kitabu cha;

**Warumi 8:18-24**

**"Nayahesabu mateso yetu ya wakati huu kuwa si kitu kulinganisha na utukufu utakaodhihirishwa kwetu.**

**Kwa maana viumbe vyote vinangoja kwa shauku kudhihirishwa kwa watoto wa Mungu.**

**Kwa kuwa viumbe vyote viliwekwa chini ya ubatili, si kwa chaguo lao, bali kwa mapenzi yake yeye aliyevitiisha katika tumaini, ili kwamba viumbe vyote vipate kuwekwa huru kutoka kwa utumwa wa kuharibika na kupewa uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu.**

**Kwa maana twajua ya kuwa hata sasa viumbe vyote vimekuwa vikilia kwa maumivu kama utungu wa mwanamke wakati wa kuzaa.**

**Wala si hivyo viumbe peke yao, bali hata sisi ambao ndio matunda ya kwanza ya Roho, kwa ndani tunalia kwa uchungu tukisubiri kwa shauku kufanywa wana wa Mungu, yaani, ukombozi wa miili yetu.**

**Kwa kuwa tuliokolewa kwa tumaini hili. Lakini kama kinachotumainiwa kikionekana hakiwi tumaini tena. Je, kuna mtu anayetumaini kupata kitu alicho nacho tayari?"**

Neno linasema; viumbe vyote (vilivyo hai na visivyo hai) vinasubiria udhihirisho wa watoto wa Mungu na kwamba hivi viumbe viliwekwa chini sio kwa mapenzi yao bali kwa mapenzi ya Mungu.

Hii inatuonyesha sisi kuwa kupitia Mungu tunayo mamlaka ya kutiisha viumbe vyote na vikafanya yale sisi tutakayo.

Kwahiyo hiki kitabu ni uwekezaji mkubwa sana katika maisha yako.

Kama utajifunza kwa moyo wa shukrani na kufanya matendo ya kiimani yaliyomo humu basi kwa muda mfupi tu utaona namna ambavyo maisha yako yatabadilika na kuchukua sura mpya.

Unatakiwa ujue kuwa maisha ya duniani hapa siku zote ni mapambano, vitu unavyovitaka hata wengine wanavitaka na kuna wenzio wanaoenda kwa waganga na kutumia vitu kukurogea lakini kwa kuwa sisi tunae Yesu tutavisemesha vitu na ninaamini vitaenda kubadilisha maisha yetu.

Mwaka 2023, nilifanya mkutano wa Signs and Tokens wa siku 6(Dar es salaam) na siku 4 (Dodoma) na kutokana na mikutano hii ziko shuhuda nyingi sana za watu ambazo Mungu aliwatendea kupitia matendo haya ya imani.

Wapo waliopata promotions, wapo waliopata kazi, wapo ambao walipona na kufunguliwa na vifungo mbalimbali.

Hivyo ninakuombea mwanangu, ukiwa unasoma kitabu hiki na kufanya matendo ya Imani yaliyomo humu Mungu akaguse

maisha yako sawa sawa na kiu yako na kila kilichokufunga kikakuachie na ukawe huru siku zote.

Wewe ni mshindi na zaidi ya kushinda; karibu usome kitabu hiki na Mungu akakusaidie uone majibu ya maombi yako. AMEN

## *Sura ya Kwanza*

### TENDO LA IMANI KWA KUTUMIA MCHANGA/ UDONGO

Tendo la imani utakalojifunza kwanza ni namna ya kuusemesha au kuiamrisha ardhi ya nchi kukutumikia. Biblia inasema katika kitabu cha;

**Isaya 42:22**

**"Lakini watu hawa ni watu walioibiwa na kutekwa; wote wamenaswa katika mashimo, wamefichwa katika magereza; wamekuwa mawindo, wala hapana aokoaye; wamekuwa mateka, wala hapana asemaye, Rudisha"**

Hapa Tunaona ya kuwa kumbe wapo watu wanaotembea duniani lakini hawajui ya kuwa wamefukiwa katika mashimo. Hawajui kama ndoa zao, familia zao, biashara zao na vipawa vyao vimefukiwa katika mashimo.

Sio ajabu wengine mlivyokuwa wadogo mlikuwa na vipaji na akili nyingi lakini ukijiangalia sasa hujioni kuwa vile ulivyokuwa unajiona. Neno la Mungu linasema; watu wameibiwa haki zao, wamefukiwa katika mashimo, vipawa na karama zao zimefukiwa katika mashimo.

Ili kupata stahiki zako tena inabidi utoke katika mashimo, lazima mashimo yafukuliwe ili wewe utoke.

Kuna baadhi ya watu picha zenu, picha za watoto wenu, na majina yenu yalipelekwa kwa waganga na yakafukiwa chini ya ardhi na kunenewa maneno mabaya ya kuzika maisha yenu.

Kama wewe usipoinenesha ardhi kwa maneno na kuomba kujitoa katika mashimo haijalishi utafanya kazi kiasi gani au utafanya nini, kama umefukiwa mpaka utakapotolewa mashimoni ndio utakapopata uhuru wako.

Kwahiyo tendo hili la imani ni kwa ajili ya kuinenesha ardhi ikafufue kila kilichofukiwa ambacho ni cha kwako. Lakini ukiachana na kuombea vitu vyako vilivyofukiwa kufufuliwa utaongea na ardhi ili ipate kukukubali na kukuridhia kwa kila kitu utakachokifanya.

Kama ni biashara basi mkoa wowote utakaoenda ukakubalike, kama ni siasa basi kila sehemu ya nchi utakayokanyaga watu wa mji huo wakakukubali, kama unataka kufungua huduma basi popote pale utakapoanzisha duniani ukapate kibali na ..........................................................................................
..............................................................................